

Tarehe 05.04.2024

**TANGAZO LA ZABUNI YA UTOAJI HUDUMA YA KISHERIA KWA KCU (1990) LTD MSIMU  
2024/2025**

Zabuni na: KCU/Z/2024/2025/06

1. KCU (1990) Ltd inahitaji huduma ya Kisheria kwa mambo mbalimbali ya kiofisi. Mambo hayo ni ya ushauri wa kisheria kama, kuandaa madai na kujibu madai yanayoletwa dhidi yake, kuiwakilisha KCU(1990) Ltd katika mahakama na mabaraza ya Ardhi na nyumba ya Wilaya.
2. Kutokana na uhitaji wa huduma ya kisheria na kwa vile KCU (1990) Ltd ni taasisi ya wananchi yenyehaki ya kushitaki na kushitakiwa, hivyo yanakaribishwa maombi ya zabuni kwa ajili ya kutoa huduma ya kisheria msimu 2024/2025.
3. Mwombaji awe na ofisi inayotoa huduma ya uwakili Bukoba Manispaa.
4. Mwombaji awe wakili aliye hitimu shule ya sheria inayotambuliwa.
5. Mwombaji awe mwanachama wa Tanganyika Law society
6. Mwombaji ataje gharama zote za kutoa huduma kisheria kuanzia na 'Retainership fee' na gharama nyingine.
7. Mwombaji awe na usajili wa TIN/VAT.
8. Mwombaji aeleze uzoefu wa kazi alizowahi kufanya.
9. Ombi la zabuni liwe na jina, anuani halisi la mwombaji na mahali Ofisi ilipo. (Physical address)
18. Maombi yaambatane na ada ya TShs. 100,000/= ambazo hazitarejeshwa kwa mwombaji. Fedha hizo zilipwe kuititia A/C Namba **01J1055955001 KAGERA COOPERATIVE UNION (1990) LTD** iliyopo CRDB
10. Tathmini itafanywa kwa kuzingatia vigezo 1-10 vilivyo tajwa hapo juu.
11. Barua za maombi zilizofungwa katika bahasha yenyehaki na kuandikwa juu yake:-  
**"MAOMBI YA ZABUNI YA UTOAJI HUDUMA YA KISHERIA MSIMU 2024/2025"** \_kwa anuani tajwa hapa chini,

MENEJA MKUU,  
KCU (1990) LTD,  
P.O BOX 5,  
BUKOBA.

12. Bahasha hiyo iletwe kwa mkono katika ofisi ya manunuzi KCU (1990) Ltd kabla au mnamo tarehe 19.04.2024. saa 4.00 asubuhi siku ya Ijumaa na ufunguzi wa maombi yote utafanyika muda huo, waombaji au wawakilishi wa waombaji wanaalikwa katika ufunguzi mara tu baada ya saa ya mwisho yakupokea zabuni
13. Maombi yatakayo chelewa, maombi yasiyokamilika, maombi yaliyowasilishwa kwa njia ya kieletroniki na maombi yasiyokuwepo siku ya ufunguzi hayatahusishwa na uchambuzi wa kumpata mzabuni.

05 APR 2024